

MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI



**MAJIBU YA MASWALI
YAKO KUHUSU VETA**

UTANGULIZI

Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) ni Wakala wa Serikali iliyoanzishwa kwa Sheria ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, Sura ya 82 ikiwa na majukumu ya utoaji, ugharamiaji na uratibu wa elimu na mafunzo ya ufundi stadi nchini.

DIRA

Tanzania yenyе mafundi stadi mahiri na wa kutosha

DHIMA

Kuhakikisha upatikanaji wa ujuzi wa Ufundi Stadi nchini Tanzania kupitia utoaji na ukuzaji wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi ili kukidhi mahitaji ya soko la ajira kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

MAADILI YA MSINGI

- i. Watu Kwanza
- ii. Ustadi na Ubunifu
- iii. Umoja na Uadilifu
- iv. Yenye Kufaa

MAJUKUMU YA VETA

- i. Kutoa Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi
- ii. Kuratibu Utoaji wa Mafunzo ya Ufundi Stadi
- iii. Kugharamia Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi

ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI HUMAANISHA NINI?

Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi ni mafunzo yanayopatia mtu ujuzi wa ufundi wa kutenda kazi na hutolewa kwa vitendo zaidi ili kumwezesha mhitimu kukidhi mahitaji ya soko la ajira.

NINI FAIDA ZA KUJIFUNZA UFUNDI STADI?

- i. Mafunzo ya ufundi stadi humuwezesha mtu kutenda kazi kwa ufanisi na kwa vitendo zaidi.
- ii. Ufundi stadi humpa mhitimu fursa pana ya ajira na kumuwezesha kuajiriwa au kujajiri.
- iii. Uhitaji wa mafundi stadi kwenye soko la ajira ni mkubwa zaidi. Mfano kwa wastani mahala penye mhandisi mmoja panahitajika mafundi stadi 25.
- iv. Kupata uzoefu wa utendaji kazi na mazingira halisi ya mahala pa kazi.

MAFUNZO HUTOLEWA KWA MUDA GANI?

MAFUNZO YA MUDA MREFU

Mafunzo ya muda mrefu hutolewa kwa muda wa miaka miwili hadi mitatu. Mwanafunzi anaweza kuhitimu mafunzo yake na kutunukiwa cheti cha kitaifa cha ufundi stadi ngazi ya pili (VC 2) ikiwa amesoma kwa miaka miwili.

Kwa wanafunzi wanaoendelea na mafunzo kwa ngazi ya tatu hutunukiwa cheti cha kitaifa cha ufundi stadi ngazi ya tatu (VC 3).

MAFUNZO YA MUDA MFUPI

Mafunzo ya muda mfupi hutolewa kwa muda wa kuanzia wiki mbili hadi miezi sita kutegemea na kozi anayosoma mhusika.

NI SIFA GANI ZINAHITAJIKA ILI KUJIUNGA NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI?

MAFUNZO YA MUDA MREFU

Baadhi ya fani zinahitaji mtu mwenye elimu kuanzia kidato cha nne na kuendelea mfano Ufundu Umeme, Ufundu Magari, Elektroniki n.k. Kuna fani zingine zinahitaji mtu mwenye elimu ya darasa la saba na kuendelea. Fani hizo ni Useremala, Upakaji Rangi, Uashi pamoja na Ubunifu, Ushonaji na Teknolojia ya Nguo.

MAFUNZO YA MUDA MFUPI

Mtu ye yote anayejua kusoma na kuandika.

JE UKISOMA UFUNDI STADI UNAWEZA KUJIENDELEZA NA NGAZI ZA JUU ZAIDI KIELIMU?

Ndiyo, mhitimu wa ufundu stadi ngazi ya tatu aliyetunukiwa cheti cha kitaifa cha ufundu stadi ngazi ya tatu (VC 3) anaweza kuijendeleza kimasomo kwenye ngazi ya nne (NTA 4) hadi sita (Diploma) na kuendelea hadi ngazi ya kumi (Shahada).

NITAJIUNGAGE NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI?

MAFUNZO YA MUDA MREFU

Fomu za maombi ya kujiunga na vyuo vya VETA hutolewa mwezi Julai hadi Septemba kila mwaka na masomo huanza mwezi Januari mwaka unaofuata.

Fomu hizo hupatikana kwenye vyuo vyote vya VETA nchini pamoja na tovuti ya VETA www.veta.go.tz.

MAFUNZO YA MUDA MFUPI

Fomu za maombi ya kujiunga hupatikana katika vyuo vya VETA na hutolewa wakati wote kulingana na uhitaji.





GHARAMA ZA MAFUNZO YA UFUNDI STADI ZIKOJE?

Ada za mafunzo ya muda mrefu kwa vyuo vinavyomilikiwa na VETA ni Shilingi 60,000/= kwa mwanafunzi wa kutwa na Shilingi 120,000/= kwa mwanafunzi wa bweni kwa mwaka katika fani zote.

Aidha, kuna gharama za mahitaji mahsusizi za mafunzo anazopaswa kuchangia mwanafunzi kulingana na fani anayosoma. Gharama hizo huwa kati ya 200,000/= hadi 250,000/= kwa mwaka.

Gharama za mafunzo ya muda mfupi hutofautiana kulingana na kozi na mahitaji ya fani husika.

NI NINI KINASABABISHA ADA ZA MAFUNZO YA UFUNDI STADI KUWA NAFUU?

Serikali hugharamia asilimia 90 ya ada na gharama za wanafunzi wanaosoma mafunzo ya muda mrefu katika vyuo vya VETA kupitia Mfuko wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VET Fund). Chanzo kikuu cha mapato ya mfuko huu ni Tozo ya Kuendeleza Ujuzi (Skills and Development Levy-SDL) ambayo waajiri huchangia.

NI JINSI GANI MTEJA ANAWEZA KUWASILISHA MALALAMIKO, HOJA AU MAONI KWA VETA?

Malalamiko, hoja au maoni kuhusu huduma zinazotolewa na VETA yanaweza kuwasilishwa kupitia njia zifuatazo:-

- i. Barua pepe: pr@veta.go.tz
- ii. Simu: 0755 267 489
- iii. Mfumo wa kuwasilisha malalamiko uliopo kwenye tovuti ya VETA: www.veta.go.tz

UFUNDI STADI KWA AJIRA NA MAENDELEO YA VIWANDA



KWA MAWASILIANO NA TAARIFA ZAIDI:

VETA Makao Makuu,

**12 Barabara ya VETA, 41104 Tambukareli,
Kiwanja Na: 18 Central Business Park (CBP)**

S. L. P. 802, Dodoma, Tanzania

Baruapepe: info@veta.go.tz

Simu: +255 22 2863409

Nukushi: +255 22 2863408

Tovuti: www.veta.go.tz

0755 267 489

info@veta.go.tz

